

UKATILI MBAYA MSUMBIJI

^{Mwafrika}
LUISE bin Kumwa wa kijiji cha Mwatidi katika Msumbiji amefika katika ofisi yetu akiwa taabani baada ya kusafiri kwa miguu kwa siku kadha toka Msumbiji wakati anatoroka toka nchi hiyo.

...Amenieleza kuwa mambo katika Msumbiji sasa hayasemekwi, Wareno wameleta majeshi ya askari Ulava na kuwasambaza kote nchini.

Zana za vita ni nyingi sana na madege yao yanaranda kila mahali katika Msumbiji.

Wananchi wanakamatwa

kwa wingi na haijulikani wanapelekwa wapi. Inadhaniwa kuwa watu wanaokamatwa wanapelekwa katika Boma la Mueda.

Jambo la kushangaza alisema bwana huyu ni kule kuvifukia visima vya maji.

Visima vya maji vinafukiwa ili watu wakose maji ya kunywa na kutumia kwa shida nyingine. Askari polisi wanawekwa njiani kuwazuia watu wasiende kuchota maji kwenye visima ambavyo havijazibwa.

20/8/62